



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. EB.318/467/01B/66



27/03/2025

**Watumishi Wote,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P. 30,
NGARA.**

YAH: TANGAZO LA MKOPO WA HAZINA.

Husika na mada tajwa hapo juu.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji imepokea mgao wa fedha kiasi cha TShs **400,000,000.00 (Milioni mia nne)** kutoka katika **Mfuko wa Mikopo wa Watumishi – Hazina** kwa ajili ya kuwakopesha watumishi wa umma kununua Magari, Samani, Matengenezo ya magari na pikipiki. Hivyo, Watumishi wote wenye sifa za kupata mkopo huo wanatangaziwa kujaza fomu ya maombi ya mkopo kwa njia ya mfumo wa “**Advances Loan System**” kupitia dirisha “**als.muse.go.tz**” kwa kuzingatia ngazi za mishahara yao kuanzia tarehe **27/03/2025** hadi **02/04/2025** saa 9:30 P.M. (Alasiri).

SIFA/VIGEZO NA MASHARTI YA KUPATA MKOPO:

1. Awe mtumishi wa fungu la 87V5 – Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.
2. Awe ameajiriwa kwa masharti ya kudumu na pensheni.
3. Awe amethibitishwa kazini.
4. Awe na 1/3 ya mshahara wake.

5. Asiwe na shauri la nidhamu.
6. Asiwe na mkopo utolewao na HAZINA.
7. Asiwe na mkopo zaidi ya mmoja kutoka katika Taasisi zingine za mikopo.

Aidha kwa wale ambao walioomba mikopo hiyo kwa awamu iliyopita na hawakufanikiwa kupata kwa kuwa namba zao hazikufikiwa hawashauriwi kuomba tena kwa sababu tayari wapo kwenye "database" hivyo watazingatiwa kulingana na namba zao zile zile ambazo ziko kwenye "database".

Mbali na tangazo hili, nimeambatanisha nyaraka inayoonyesha hatua za kufuata unapoomba mkopo kwa njia ya mfumo wa Hazina Portal na maombi yote yatapokelewa kwa njia ya mfumo pekee.

Nawatachia utekelezaji mwema,


Josephat M. Sangatati

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NGARA



HATUA ZA KUJISAJILI NA KUOMBA MKOPO WA SERIKALI

1. Nenda kwenye chrome uandike als.muse.go.tz halafu bofра “enter”.
2. Itakuletea uwanja wa User name na Password usiandike chochote nenda verify ya register bofya hapo,
3. Itakuletea uwanja kujaza taarifa zako, jaza kwa usahihi halafu “verify details”.
4. Itakuletea uwanja mwingine hakiki taarifa bofya neno “Continue with Registration”.
5. Itakuletea Uwanja mwingine jaza taarifa tena kwa usahihi kasha bofta “NEXT”.
6. Itakuletea uwanja mwingine tengeneza password na urudie kuijaza (Confirm password).
7. Bofya Register.
8. Angalia kwenye email yako utabofya “verify email”.
9. Itakuletea uwanja mwingine utabofya “proceed phone verification”.
10. Utatumwa CODE kwenye namba yako ya simu uliyoijaza utazicopy na kuzipaste kwenye vibox halafu utabodya “verify”.
11. Utarudi kwenye page na kuandika User name (Check namba) utajaza na password uliyoitengeneza halafu utabodya “Log in”.
12. Utabofya “Advance loan” upande wa kushoto.
13. Utabofya neno “Apply” upande wa kulia halafu utajaza taarifa zinazohitajika.
14. Utajaza kiasi cha mkopo unaohitaji kwenye (Request amount).
15. Utajaza miezi unayotaka kurejesha mkopo zaidi ya miezi 72 kwenye (Recover period).
16. Utabofya “Submit”.
17. Utabodya vidoti vitatu vinavyoonyesha upande wa kulia kwenye Action.
18. Utabodya neno “More details” halafu utabodya neno “Submit” upande wa kulia juu kwenye remark utakuwa umesubmit kwa mwakilishi wa mkopo na hapo utakuwa umekamilisha usajiri na umeomba Mkopo wa Serikali kwa hiyo status itakuwa inaseomeka (Application Submitted) na stage itasomeka (Submitted to Loan Representative).
19. Baada ya mkopo wako kuidhinishwa unatakiwa kupakua mkataba wa mkopo kwenye mfumo, usaini sehemu zote mbili (02) zinazokuhusu, na kuusainisha kwa Mkurugenzi na kugongwa mhuri baada ya kusainiwa pakia fomu yako kwenye mfumo na kuirejesha (Submit) kwa mwailishi wa Mikopo (Loan Representative).
20. Hakikisha unatembelea akaunti yako mara kwa mara kwa ajili ya kukamilisha maombi yako ya mkopo kama utakuwa miiongoni mwa watumishi waliokubaliwa/kuidhinishiwa kukopa mkopo huu.